# KIJARIDA CHA KUJIELIMISHA JAMII JUU YA MASUALA MUHIMU YA HAKI ZA ARDHI KWA

# WANAWAKE NCHINI TANZANIA

HAKIARDHI Vol.4. Januari,2018 LandRightsResearch&ResourcesInstitute



## UTANGULIZI

Sera na Sheria mbalimbali nchini Tanzania zinatoa fursa kwa makundi yote kuwa na haki ya kupata, kutumia, kumiliki na kunufaika na rasilimali mbalimbali ikiwemo ardhi. Kijarida hiki kinachambua Sera na Sheria hizi hasa kikiangazia haki za ardhi kwa kundi kubwa la wanawake, kama ifuatavyo;

### 1. Haki ya kumiliki mali

Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977(kama ilivyorejelewa mara kwa mara) inaainisha ya kuwa kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria. Hivyo Wanawake na Wanaume wana haki sawa katika kumiliki ardhi kama mojawapo ya mali.

### 2. Haki ya mwanamke kupata ardhi

Kifungu cha 3(2) cha Sheria za Ardhi namba 4 na 5 kinaainisha ya kwamba haki ya kila mwanamke kupata, kumiliki, kutumia na kuuza au kuigawa ardhi ifahamike kuwa ni sawa sawa na haki ya mwanaume yoyote kwa viwango vilevile na masharti yale yale. Halikadhalika kifungu cha 23(2)(c) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 kimeainisha kwamba katika kupitisha uamuzi kuhusu maombi ya hakimiliki ya kimila Halmashauri ya Kijiji inapaswa kuzingatia maombi ya wanawake sawa sawa na maombi ya wanaume.

### 3. Ulinzi wa mali ya familia dhidi ya rehani

Kifungu cha 114 cha Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999, kimetoa ulinzi kwa mali ya familia kuwekwa rehani kwa kuainisha kwamba rehani ya nyumba ya familia itakuwa halali endapo itakuwa na saini inayoonesha Mke au Wake kuridhia uwekaji wa rehani wa nyumba hiyo. Vile vile kifungu cha 8 cha Sheria ya Rehani namba 17 ya mwaka 2008, kinazungumzia wajibu wa Mkopaji kumjulisha Mkopeshaji kuwa ana Mke na ameoa, hivyo ni muhimu kwa Mkopaji kutoa taarifa kuwa yeye ana Mke au Mume. Pia Sheria inatamka kuwa ni kosa la jinai kudanganya kuwa Mkopaji hana Mke na anaweza kufungwa kwa muda wa miezi 12 au kulipa faini isiyopungua nusu ya thamani ya mkopo endapo itabainika kuwa alidanganya.

### 4. Haki ya mwanamke kwenye umiliki wa ardhi pamoja

Kifungu cha 161(1) na (2) cha Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999, kinaruhusu umiliki wa ardhi pamoja na kumlinda Mwanamke katika umiliki wa aina hiyo. Vilevile kama ardhi hiyo ilikuwa inamilikiwa katika jina la Mwanaume na Mke wake ameweka nguvu zake katika kuzalisha na kuiboresha ardhi hiyo basi Mwanamke anapata hadhi sawa ya umiliki hata kama jina lake halijaandikwa katika hati au cheti cha hakimiliki ya kimila.

### 5. Ulinzi wa ardhi ya familia dhidi ya uuzwaji

Kifungu cha 161(3) cha Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999, kinaainisha kwamba kabla ya uuzwaji wa ardhi ya familia ni jukumu la mnunuzi kujiridhisha kuwa ridhaa ya mke au wake halali imepatikana. Vilevile kifungu hicho kina ainisha ya kuwa kama uuzwaji wa ardhi hiyo unatokana na rehani ni jukumu la Mkopeshaji kujiridhisha kuwa Mke au Wake halali waliridhia rehani hiyo.

### 6. Ulinzi dhidi ya mila kandamizi

Kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 kinaainisha kwamba matumizi ya mila na desturi zinazowanyima wanawake, watoto au watu wenye ulemavu njia halali za kumiliki, kukalia au kutumia ardhi ni batili na hazitatumika na kutekelezwa katika vyombo ya usimamizi wa ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini.

### 7. Haki ya uwakilishi katika Kamati ya Maamuzi ya Kijiji

Kifungu cha 53(2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 kinaainisha kwamba Kamati ya Maamuzi ya Kijiji itaundwa na wajumbe wasiozidi 9 kati yao wajumbe wasiopungua 4 ni lazima wawe wanawake.

### 8. Haki ya uwakilishi katika Baraza la Ardhi la Kijiji

Kifungu cha 60(2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 pamoja na kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Mabaraza na Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi namba 2 ya mwaka 2002 vimeainisha kuwa Baraza la Ardhi la Kijiji litaundwa na wajumbe 7 kati yao idadi ya wanawake haitakiwi kupungua 3.

### 9. Haki ya uwakilishi katika Baraza la Kata

Kifungu cha 11 cha Sheria ya Mabaraza na Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi namba 2 ya mwaka 2002 pamoja na kifungu cha 4 cha Sheria ya Mabaraza ya Kata, namba 7 ya mwaka 1985 vimeainisha kuwa Baraza la Kata litaundwa na wajumbe wasiozidi 8 na wasiopungua 4 ambapo idadi ya wanawake haitakiwi kupungua 3.

### 10. Haki ya uwakilishi katika vyombo vinavyosimamia ardhi kijijini

***(i) Halmashauri ya Kijiji***

Kwa mujibu wa kifungu cha 56(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) namba 7 ya mwaka 1982 idadi ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji inatakiwa isipungue 15 na isizidi 25 kati yao idadi ya wanawake haitakiwi kupungua robo ya wajumbe wote.

***(ii) Mkutano Mkuu wa Kijiji***

Kwa mujibu wa kifungu cha 55 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) namba 7 ya mwaka 1982, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa kijiji ni wakazi wote wa kijiji wenye umri usiopungua miaka 18 na wenye akili timamu bila kujali jinsia.

### 11. Haki ya kumiliki ardhi baada ya talaka

Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa namba 5 ya mwaka 1971 mgawanyo wa mali za ndoa ikiwemo ardhi wakati wa talaka unategemea aina ya ndoa iliyofungwa na wanandoa. Zipo aina 3 za ndoa ambazo ni ndoa ya kimila, kidini na kiserikali. Mgawanyo wa mali wakati wa talaka kwa taratibu za ndoa za kidini na kiserikali unatoa haki kwa wanawake kupata mali ya ndoa kulingana na aina ya ndoa, mchango wa wanandoa na maamuzi ya mahakama. Mgawanyo wa mali za ndoa kwa taratibu za ndoa za kimila unategemea mila na desturi za jami husika. Uzoefu unaonesha kuwa mara nyingi wanawake wanakosa haki ya kupata mgawanyo sawa na wanaume kutokana na mila na desturi nyingi kuwa kandamizi.

### 12. Haki ya wanawake katika mirathi

Mirathi ni utaratibu wa namna mali ya marehemu itakavyogawiwa kwa warithi wake. Mgawanyo wa mirathi nchini unaongozwa na sheria tatu za mirathi ambazo ni; Sheria ya Kimila (Tamko la Sheria za Kimila namba 4 la mwaka 1963), Sheria ya Kiislam (The Islamic Law (Restatement) Act, 1964 na Sheria ya Kiserikali (The Probate and Administration of Estates Act).

***(i) Mgawanyo wa Mirathi kwa Sheria ya Kimila***

Sheria ya kimila inayotumika kugawa mirathi imetokana na mila na desturi za jamii husika zilizokusanywa katika makabila yanayorithi kufuata ukoo wa baba ambayo ni zaidi ya asilimia 85 ya makabila yote.

- Watanzania wote ambao ni wazawa wasio na asili ya kiasia, kizungu, au kisomali hutumia sheria hii katika mirathi yao.
- Kama ikithibitika kuwa mzawa aliacha kabisa mila na desturi za kabila lake wakati wa uhai wake Sheria ya Kiislam itatumika kugawa mali zake kiislamu kama marehemu alikuwa Muislam. Kama marehemu hakuwa Muislam Sheria ya Kiserikali itatumika kugawa mirathi.

Mgawanyo wa mali katika Sheria ya Kimila umepangwa katika madaraja matatu kama ifuatavyo;

a) Daraja la I- Mtoto wa kwanza wa kiume wa ndoa ya kwanza hurithi sehemu kubwa kuliko warithi wengine.

b) Daraja la II- Watoto wa kiume wote waliosalia ambao hupata fungu dogo ukilinganisha na mrithi wa Daraja la I.

c) Daraja la III- Watoto wa kike wote bila kujali nafasi na umri, hawa hupata fungu dogo kuliko warithi wote.

**ZINGATIA**

(i) Katika Sheria za Kimila mjane hana fungu katika urithi bali hutegemea watoto kumtunza.

(ii) Watoto waliozaliwa nje ya ndoa hawarithi kwa baba yao isipokuwa pale ambapo wanakuwa wamehalalishwa kwa kufuata mila na desturi za jamii husika, vinginevyo hurithi upande wa mama.

(iii) Sheria ya Kimila pia inafafanua kuwa mtoto wa nje ya ndoa hata kama amehalalishwa na wakati mwingine ni mkubwa kuliko yule aliyezaliwa kwenye ndoa hawezi kuwa mrithi Daraja la I.

(iv) Kesi zinazohusu kugawa mali ya marehemu kwa Sheria ya kimila lazima zifunguliwe katika Mahakama ya mwanzo.

***(ii) Mgawanyo wa Mirathi kwa Sheria ya Kiislam***

Sheria ya Kiislam inatumika kugawa mirathi kwa Watanzania wote ambao itathibitika kuwa wameacha mila na desturi zao na ambao Uislam huwaongoza katika vipengele vyote vya maisha yao pamoja na watu wale ambao si wazawa ila ni waislam.
Mgawanyo wa mirathi kwa Sheria ya Kiislam ni kama ifuatavyo;

a) Wajane/Mjane hurithi 1/8 kama marehemu ameacha watoto.

b) Wajane/Mjane hurithi ¼ kama marehemu hakuacha watoto.

c) Wazazi hupewa $^1/_6$ ya salio baada ya kuondoa fungu la mjane/wajane.

d) Mali iliyosalia hugawanywa katika mafungu matatu ambapo watoto wa kiume hupata mafungu mawili na wa kike fungu moja.

e) Mgane hupewa ¼ ya mali ya marehemu mke wake kama kuna watoto au ½ kama hakuna watoto.

**MUHIMU:** Mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa hawezi kurithi mali ya Baba yake kwa Sheria ya Kiislam labda kama marehemu ameacha wosia.

***(iii) Mgawanyo wa Mirathi kwa Sheria ya Kiserikali***

Sheria ya Kiserikali (The Probate and Administration of Estates Act) hutumika na Watanzania walioacha mila na desturi zao pamoja na watu wengine ambao si wazawa na wala si Waislam.

Mgawanyo wa urithi katika Sheria ya Kiserikali ni kama ifuatavyo:

***1. Marehemu akiacha watoto***

- $^1/_3$ hurithiwa na mjane/mgane.
- $^2/_3$ hugawiwa sawasawa kwa watoto wote.

***2. Marehemu hakuacha watoto***

- ½ hupata mjane/mgane.
- ½ hupata wazazi wa marehemu au ndugu wa karibu iwapo wazazi hawapo.

***(iv) Taratibu za kufungua mirathi***


**Wosia ukiwepo;**

a) Mtu anapofariki kifo kiandikishwe katika ofisi ya vizazi na vifo katika wilaya husika ndani ya muda wa siku 30 tangu kifo kutokea.

b) Endapo wosia haukumtaja msimamizi wa mirathi japokuwa si utaratibu wa kisheria mkutano wa ukoo ufanyike na kupendekeza msimamizi wa mirathi.

c) Msimamizi aliyependekezwa au kutajwa katika wosia afungue mirathi katika mahakama ya mwanzo iwapo sheria itakayotumika ni ya kimila au ya kiislam akiwa na nakala ya muhtasari wa kumbukumbu za kikao cha ukoo na cheti cha kifo.

Ukoo au ndugu wa marehemu hutoa mapendekezo tu juu ya mtu anayefaa kuwa msimamizi wa mirathi lakini ni mahakama pekee yenye uamuzi wa mwisho.




***Wosia usipokuwepo;***

a) Mtu anapofariki kifo kiandikishwe katika ofisi ya vizazi na vifo katika wilaya husika ndani ya muda wa siku 30 tangu kifo kutokea.

b) Mkutano wa ukoo ufanyike kumpendekeza msimamizi.

c) Msimamizi aliyependekezwa aende kufungua mirathi mahakamani akiwa na nakala ya muhtasari wa kumbukumbu za kikao cha ukoo na cheti cha kifo.

d) Mahakama hutoa tangazo la mirathi kwa muda wa siku 90 kama hakuna pingamizi lolote msimamzi hukabidhiwa barua za usimamizi wa mirathi.

e) Msimamizi anatakiwa kugawa mirathi kwa mujibu wa sheria, kufuatana na maisha aliyoishi marehemu.

**ZINGATIA:** Mirathi hufunguliwa kufuatana na makazi ya marehemu.

care

HAKIARDHI

**KWA MAWASILIANO ZAIDI TUMIA ANUANI ZIFUATAZO**
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi –HAKIARDHI
Kitalu Na.236 Block 47 Sinza Mori, S.L.P 75885, Dar es Salaam,
Simu +255 22 2771360/ 0784 646752, Nukushi: +255 22 2771362,
Baruapepe: info@hakiardhi.org, Tovuti: www.hakiardhi.org